


Tanzanian delegates to the SADC (Southern African Development Community) meeting for permanent secretaries under whose ministries the disaster management docket most directly falls follow proceedings at the opening of the event in Zanzibar yesterday. From L: Dr Faraji Mnyepe (Defence and National Service), Prof Elisante ole Gabriel (Livestock and Fisheries) and Christopher Kadio (Home Affairs). Photo: Ibrahim Hamidu

## ... records decline in road crashes

## Ra... to...

By Gua...

TRU... for fo... forest... tance... in Ki... Distr... secor... child...

Th... Ward... to th... build...

Jo... resid... them... scho... stud... Seco... quir... fore...

## G... en...

By ...

I... ce... to... pr... fri...

ity... try... ex...

The Guardian

# Herders cry foul after losing 1,400 impounded cattle

FROM PAGE 1

to get them back, but after paying the fine he was not handed back his animals.

Alex Ngulukulu, the secretary of Itilima MP Njalu Daudi Silanga (CCM), speaking on behalf of the herders, said forest reserve officials said 289 cattle had died which he said was not true.

Some forest reserve officials were known to have been conducting cattle auctions inside the reserve while the case was still in court, and the herders have evidence for the sales, including auction receipts, he declared.

Tindabuligi ward councillor Tabu Maghembe said they do not subscribe to the argument that the cattle perished as there was no eruption of any cattle diseases reported during the period. He appealed to the minister to convey their grievances to President John Mafufuli.

The herders also complained over the decision by forest reserve officials to expand the reserve area without consulting residents in the area, thereby reducing the size of their grazing areas.

Juma Mpina, the vice-chairman of the Meatu District Council expressed gratitude to President Magufuli for adding 500 metres of grazing land by shifting the Maswa Forest Reserve boundary as well 60 metres reduced from river banks reserved area and allowing the cattle to drink water on the banks of the river.

In the past they did not have this dispensation resulting in many of their animals dying, he said.

The minister directed Meatu and Itilima district commissioners to convene a joint meeting that will involve the Maswa Forest Reserve Chief Conservator, the Director of Livestock Services in the ministry, the ministerial Chief Legal Officer and the aggrieved herders to go through the court judgment so that justice prevails.

He also directed the Commissioner for Lands, the Director of Fisheries and the Iramba and Meatu district executive directors to go through the reserve demarcation in order to solve the conflict involving fishing in Lake Kitangiri.

Herders whose seized cattle were ordered by the court to be returned must submit their documents and other exhibits to the Itilima and Meatu DCs so that they can be examined to provide the basis for a just solution to the matter, he added.



Abo
(5th-
com

M

FR

bu
Yo
of
pl
Th
pa
m

Scanned by CamScanner

# Utata vifo ng'ombe 1,400 hifadhini Maswa

**Na Mwandishi Wetu,** SIMIYU

ZAIDI ya ng'ombe 1,400 wa wafugaji wa Wilaya za Itilima na Meatu mkoani Simiyu wamekufa katika mazingira yenye utata mikononi mwa maofisa wa Pori la Akiba la Maswa.

Inadaiwa walikufa baada ya kushikiliwa hifadhini kwa miaka mitatu bila kupatiwa huduma muhimu za chanjo, dawa, maji na malisho licha ya Mahakama kutoa hukumu kwa wamiliki kurejeshewa mifugo yao.

Wafugaji hao wamesema tangu mwaka 2017, ng'ombe 1, 484 walikamatwa kwa madai kuwa walikuwa ndani ya pori hilo, na kwamba licha ya Mahakama kuamuru warudishiwe ng'ombe wao, waliendelea kushikiliwa na kuendelea kufa na kubaki 72, hivyo kuwasababishia umasikini mkubwa.

Wafugaji hao walifikisha kilio hicho kwenye mikutano wa hadhara ilioitishwa na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, aliyefika katika vijiji vya Laini 'A' na Laini 'B' wilayani Itilima, Mwangudo na Malwilo wilayani Meatu mkoani Simiyu ambapo walisema licha ya Mahakama kutoa uamuzi wafugaji hao warejeshewe mifugo, hawajarudishiwa, na kwamba inadaiwa imekufa.

Miongoni mwa wamiliki wa mifugo hiyo ni walioshinda kesi kwa upande wa Itilima ni Malimi Sendama, Ngasa Mbeho, Kongwa Tulutu na Maduhu Mbuli, ambao walimkabidhi Waziri Mpina risiti zinazooonesha mifugo hiyo kuuzwa kwa bei ya kutupa, huku ngombe anayetakiwa kuuzwa kwa Sh. 400,000 hadi Sh. 500,000 akiuzwa Sh. 100,000.

Wafugaji wengine kwa upande wa Meatu waliodhulumiwa ng'ombe 345 ni Subi Maduhu, Masunga Muhamali, Zengo Kusekelwa, Kija Badila, ambao mifugo yao inadaiwa kufa huku mfugaji mwingine akidai ng'ombe wake 55 ambao Mahakama iliamuru alipe faini ya Sh. milioni 1.4 ili arudishiwe mifugo yake na kulipa faini hiyo, lakini mifugo yake haijarudishwa.

Akiwasilisha kilio kwa niaba ya wafugaji hao, Katibu wa Mbunge wa Itilima, Alex Ngulukulu, alisema wahifadhi hao walitoa maelezo kuwa ng'ombe 289 wamekufa, wakati si kweli kwani askari wa hifadhi walikuwa wanaendesha minada ya kuuza mifugo hiyo.

"Ng'ombe walikuwa wanauzwa kwenye minada wakati kesi ikiendelea mahakamani na tuna ushahidi wa kutosha wa risiti zote walizokuwa wanatoa kwa wanunuzi wa mifugo hiyo," alisema Alex.

Diwani wa Kata ya Tindabuligi, Tabu Maghembe, alisema maelezo yaliyotolewa kwamba mifugo hiyo imekufa hawakubaliani nayo kwani hakuna mlipuko wowote wa magonjwa ulioripotiwa katika kipindi hicho, hivyo kumuomba Mpina kufikisha kilio hicho cha wafugaji wa Itilima na Meatu kwa Rais John Magufuli ili aingilie kati kupata haki yao.

Aidha, wafugaji hao walilalamikia kitendo cha maofisa wa Pori la Akiba Maswa kutanua mpaka bila kuwashirikisha wananchi, hivyo kuendelea kupunguza eneo la malisho na kusababisha usumbufu mkubwa kwa wafugaji.

Pia wananchi wa wilaya za Maswa na Meatu wamelalamikia mgogoro wa mpaka katika Ziwa Kitangiri, na kwamba wamekuwa wakizuiliwa kuvua na kukamatwa kwamba wameingia wilaya ya Iramba Mkoa wa Singida.

Akizungumza baada ya malalamiko hayo Waziri Mpina aliwaagiza Wakuu wa Wilaya za Itilima na Meatu kuitisha kikao cha pamoja kitakachomhusisha Mhifadhi Mkuu wa Pori la Maswa, Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo Tanzania na Mwanasheria wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi na wafugaji wanaolalamikia kudhulumiwa mifugo yao. Aliwataka kupitia vielelezo vyote vilivyotumika kukamata, kutunza na kuuza mifugo pamoja na kupitia hukumu ya Mahakama ili haki iweze kutendeka .

Pia alimuagiza Kamishna wa Ardhi, Mkurugenzi wa Uvuvi Tanzania, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Meatu na Mkurugenzi wa Iramba kupitia upya mipaka hiyo na kumaliza kabisa mgogoro huo kuhusu uvuvi katika Ziwa Kitangiri

Waziri Mpina ameagiza wafugaji wote mkoani Simiyu walioshinda kesi mahakamani na kutakiwa kurejeshewa mifugo yao kuwasilisha vielelezo vya hukumu za kesi hizo kwenye ofisi za Wakuu wa Wilaya za Itilima na Meatu ili haki iweze kutendeka.


**KUPOTEA KWA CHETI**



**ZAWADI WILLIUM HAONGA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.2925-0231 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia NALYELYE SEKONDARI mwaka 2015.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**TANGAZO.**


Scanned by CamScanner

VIGOGO>> Hivi karibuni Chadema imeondokewa na Lowassa, Sumaye na Dk. Mashinji

# Mwisho magogo kukatia nyama buchani wawadia

**ASHURA ASSAD Na ATHNATH MKIRAMWENI**

WIZARA ya Mifugo kupitia Bodi ya Nyama (TMB), nchini imerudia kutoa onyo dhidi ya matumizi ya magogo katika kukatia nyama mabuchani, na kusema kuanzia Jumatatu itapita bucha hadi bucha kufanya ukaguzi wa kina.

Imesema inachukua hatua hizo kuhakikisha kila kipande cha nyama kinachouzwa au kutolewa kwa ajili ya matumizi ya binadamu kinazingatia usalama wa kiafya huku ikisema matumizi ya magogo yana athari kiafya.

Akizungumza na Uhuru jana, Dar es Salaam, Msajili wa Bodi ya Nyama, Imani Sichalwe, alisema kwa sasa mtu yeyote anayetumia magogo buchani anafanya makosa na hatua za kisheria dhidi yake zinapaswa kuchukuliwa.

Msajili huyo alisema kwa wale wanaodai wamepewa barua ya kuendelea kutumia magogo jambo hilo halina ukweli kwa sababu muda uliotolewa umepita.

> Gharama za ununuzi wa mashine ni kubwa kuliko uwezo au kipato tunachokizalisha, tunaiomba serikalia kuangalia namna ya kushusha bei ili kila mtu aweze kuzimudu.

**MSAKO MKALI**

Sichalwe alisema kuwa wanatarajia kuanza operesheni ya kusaka mabucha yanayoendelea kutumia magogo kukatia nyama nchini kuanzia Februari 24, mwaka huu, katika majiji ya Dar es Salaam, Mwanza, Mbeya, Arusha na Tanga.

Alisema kabla ya kuanza operesheni hiyo Febriari 19 (leo), wanatarajia kukaa kikao na Shirika la Viwango (TBS) na Halmashauri zote za mikoa kwa ajili ya kuangalia namna watakavyoweza kufanikisha operesheni hiyo.

"Hatujashindwa kufanya operesheni kwa mabucha ya nyama yanayotumia magogo, tunachokitarajia ni kukaa kikao na TBS na Halmashauri zote za mikoa kwa ajili ya kuangalia namna tutakavyoweza kufanikisha operesheni hiyo," alisema.

**MTAZAMO WA MABUCHA**

Wakizungumza kwa nyakati tofauti jijini Dar es Salaam, baadhi ya wafanyabiashara ya nyama hususan katika eneo la Kariakoo, akiwemo Isihaka Rashidi, alisema wako tayari kutumia mashine za kukatia nyama na kuachana na magogo endapo mashine hizo zitauzwa kwa gharama nafuu.

"Gharama za ununuzi wa mashine ni kubwa kuliko uwezo au kipato tunachokizalisha, tunaiomba serikalia kuangalia namna ya kushusha bei ili kila mtu aweze kuzimudu," alisema.

Hamisi Jumaa mfanyabiashara wa nyama eneo la Kinondoni, alisema hatua inayochukuliwa na kulinda afya ya mlaji ni nzuri, lakini aliomba gharama za mashine zipungue ili waweze kumudu.

Alisema mashine hizo zinauzwa kwa sh. millioni 1.5 na kuendelea kiasi ambacho wengi wao kinakuwa kigumu kukimudu.

**ATHARI KWA NYAMA ILIYOKATWA KWA GOGO**

Akitoa ufafanuzi, Sichalwe alisema nyama inayouzwa kwenye mabucha yasiyotumia misumeno na mashine si salama kwani inaweza kumletea madhara ya kiafya mlaji kwa kuwa magogo hayo yanahifadhi vimelea vya maradhi.

Alisema vimelea hivyo hutokea kwa kuwa gogo halisafishiki vyema hivyo vijidudu kuendelea kubaki.

"Hakuna namna yoyote ambayo gogo linaweza kusafishwa na kuondoa uchafu wa kutwa nzima, hapo ndipo vijidudu vinapopata nafasi na nyama inapowekwa vinahamia huko, ndio sababu tunasema ni hatari kwa afya," alisema.

Alisema vipande vidogo vya gogo vinavyotoka wakati shoka linapogonga mfupa, huingia kwenye nyama na kuiondoa kwenye usalama.

Alisisitiza walaji kutazama usalama wao wanapofanya uamuzi wa kununua nyama mabuchani ili kutoruhusu nyama inayoweza kuwaletea madhara.

Sichalwe alisema kwa muda mrefu, bodi imekuwa ikiwaelimisha na kuwaagiza wenye mabucha kutumia mashine lakini bado wapo baadhi wanaokiuka agizo hilo.

Kwa mujibu wa Sichalwe agizo hilo ni hatua mojawapo ya kuhakikisha Watanzania wanakula nyama kama inavyoelekezwa na Shirika la Chakula Duniani (FAO).

**KWA UPANDE WA TAKWIMU**

Alisema takwimu zinaonyesha kuwa licha ya Tanzania kuwa na idadi kubwa ya mifugo na kuzalisha nyama nyingi, wastani wa ulaji wa nyama ni kilo 15 kwa mwaka wakati FAO inaelekeza kilo 50 huku bodi ikibaini kuwa moja ya sababu ni gharama ya kitoweo hicho.

Pamoja na mashine za kukatia, bodi hiyo imeweka nguvu katika kuhamasisha matumizi ya mizani ya kidijitali ili kuwawezesha wateja kununua nyama kulingana na viwango vya fedha walizonazo.

"Kwenye mabucha ya kawaida bei ya nyama inaanzia sh. 5,000 hadi sh. 8,000 sasa kwa mwenye kipato kidogo anaweza kushindwa kumudu ndio sababu tunataka itumike mizani ya dijitali ili sasa nyama ipimwe kulingana na fedha aliyonayo mhitaji.

Ni muhimu kwa binadamu kula nyama kwani ina umuhimu mkubwa mwilini kutokana na viini lishe vya kipekee ambavyo kitoweo hicho inavyo ambavyo havipatikani kwenye mboga nyingine," alisema.

Sichalwe alisema nyama salama inaanzia kwenye ufugaji ambapo mfugaji anatakiwa kufuata kanuni na taratibu za ufugaji, kusafirisha mifugo kwa kuzingatia viwango na kuchinjwa katika machinjio zilizokidhi vigezo.

"Nyama bora ni ile inayotokana na mifugo iliyotunzwa kwa kuzingatia viwango vya uzalishaji bora, pia nyama inatakiwa iuzwe kwenye mabucha yaliyokidhi vigezo, usile nyama ya mezani au inayotembezwa mtaani,".

Mapema Septemba 30, mwaka jana bodi ya nyama nchini ilitangaza kuwa siku ya mwisho kwa matumizi ya magogo ya kukatia nyama mabuchani na kwamba wanatarajia kuanza operesheni kali ambapo hatua kali za kisheria zitachukuliwa kwa watakaobainika.

# wa Mashinji kutimka Chadema

Scanned by CamScanner

# *Ng'ombe 1,400 walioamriwa kurudishiwa wafugaji wafa

**Na Mwandishi Wetu, Simiyu**

ZAIDI ya ngiombe 1, 400 wa wafugaji wa Wilaya za Itilima na Meatu mkoani Simiyu wamekufa mikononi mwa Maofisa wa Pori la Akiba la Maswa baada ya kushikiliwa hifadhini kwa kipindi cha miaka mitatu bila kupatiwa huduma muhimu za chanjo, dawa, maji na malisho licha ya Mahakama kutoa hukumu kwa wamiliki kurejeshewa mifugo yao.

Wafugaji hao wamesema tangu mwaka 2017 ng'ombe 1, 484 walikamatwa kwa madai kuwa walikuwa ndani ya pori hilo na kwamba licha Mahakama kuamuru warudishiwe ng'ombe wao bado waliendelea kushikiliwa na kuendelea kufa na kubaki 72 na kuwasababishia umasikini mkubwa.

Wafugaji hao walifikisha kilio hicho kwenye mikutano wa hadhara iliotishwa na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina aliyefika katika vijiji vya Laini 'A' na Laini 'B' wilayani Itilima, Mwangudo na Malwilo Wilayani Meatu mkoani Simiyu ambapo walisema licha ya Mahakama kutoa uamuzi wafugaji hao warejeshewe mifugo bado hawajarudishiwa mifugo yao hadi sasa na kwamba inadaiwa kuwa mifugo hiyo imekufa.

Baadhi ya wamiliki wa mifugo hiyo ni walioshinda kesi kwa upande wa Itilima ni Malimi Sendama, Ngasa Mbeho, Kongwa Tulutu na Maduhu Mbuli ambapo walimkabidhi Waziri Mpina risiti mbalimbali zinazoonesha mifugo hiyo kuuzwa kwa bei ya kutupa huku ngombe anayetakiwa kuuzwa laki 4 hadi 5 akiuzwa sh laki 1.

Wafugaji wengine kwa upande wa Meatu waliodhulumiwa ng'ombe 345 ni Subi Maduhu, Masunga Muhamali, Zengo Kusekelwa, Kija Badila ambapo mifugo yao inadaiwa kufa huku mfugaji mwingine akidai ngombe wake 55 ambao Mahakama iliamuru alipe faini ya shilingi milioni 1.4 ili arudishiwe mifugo yake na alilipa faini hiyo lakini mifugo yake haijarudishwa hadi sasa.

Akiwasilisha kilio kwa niaba ya wafugaji hao, Katibu wa Mbunge wa Itilima, Alex Ngulukulu alisema wahifadhi hao walitoa maelezo kuwa ngiombe 289 wamekufa jambo ambalo sio la kweli kwani askari wa hifadhi walikuwa wanaendesha minada ya kuuza mifugo hiyo.

"Ng'ombe walikuwa wanauzwa kwenye minada wakati kesi ikiendelea mahakamani na tuna ushahidi wa kutosha wa risiti zote walizokuwa wanatoa kwa wanunuzi wa mifugo hiyo," alisema Alex.

Diwani wa Kata ya Tindabuligi, Tabu Maghembe alisema maelezo yaliyotolewa kwamba mifugo hiyo imekufa hawakubaliani nayo kwani hakuna mlipuko wowote wa magonjwa ulionpotiwa katika kipindi hicho na hivyo kumuomba Waziri Mpina kufikisha kilio hicho cha wafugaji wa Itilima na Meatu kwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli ili aingile kati waweze kupata haki yao kwani kwa muda mrefu amekuwa akipigania haki za wanyonge.

Mbali na malalamiko hayo pia wafugaji hao walilalamikia kitendo Maofisa wa Pori la Akiba Maswa kutanua mpaka bila kuwashirikisha wananchi na hivyo kuendelea kupunguza eneo la malisho na kusababisha usumbufu mkubwa kwa wafugaji. Pia wananchi wa Wilaya za Wilaya za Maswa na Meatu wamelalamikia mgogoro wa mpaka katika Ziwa Kitangiri na kwamba wamekuwa wakizuiliwa kuvua na kukamatwa kwamba wameingia wilaya ya Iramba Mkoa wa Singida.

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Meatu, Juma Mpina amshukuru Rais Dkt. John Magufuli kwa kuruhusu matumizi ya mita 500 kutoka kwenye Pori la Akiba la Maswa yatumike kwa shughuli za kulishia mifugo sambamba na kuruhusu matumizi ya mita 60 kutoka kwenye mto kutumika kwa shughuli za akunyesha maji mifugo yao jambo ambalo hapo kabla wananchi walikuwa wakizuiliwa na kusababisha mifugo mingi kufa kwa kukosa maji na malisho.

Akizungumza baada ya malalamiko hayo Waziri Mpina aliwaagiza Wakuu wa Wilaya za Itilima na Meatu kuitisha kikao cha pamoja kitakacho mhusisha Mhifadhi Mkuu wa Pori la Maswa, Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo Tanzania na Mwanasheria wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Wafugaji wanaolalamikia kudhulumiwa mifugo yao na kupitia vielelezo vyote vilivyotumika kukamata, kutunza na kuuza mifugo pamoja na kupitia hukumu ya Mahakama ili haki iweze kutendeka.

Pia ameagiza Kamishna wa Ardhi, Mkurugenzi wa Uvuvi Tanzania, Mkurugenzi wa Halmashauri y Meatu na Mkurugenzi wa Iramb ili kupitia upya mipaka hiyo n kumaliza kabisa mgogoro hu kuhusu uvuvi katika Ziwa Kitangi

Kuhusu suala la kutanua mpak kiholela, Waziri Mpina ameag timu ya Wataalamu kutoka Wiza nane kupita kwenye maene yanayolalamikiwa na kupima up mipaka hiyo kwa uwazi na kwamb wananchi watashiriki katika zoe hilo. Aidha kuhusu upungufu maeneo ya malisho vijiji sal vinavyounda WMA ya Maka Waziri Mpina aliagiza wafan tathmini ya mahitaji ya ardhi wananchi kwa sasa na kuanc GMP itakayoruhusu baadhi maeneo kutumika kwa ajili kulishia mifugo.

Hivyo Waziri Mpina ameag wafugaji wote mkoani Sim walioshinda kesi mahakamani kutakiwa kurejeshewa mifugo kuwasilisha vielelezo vya huk za kesi hizo kwenye ofisi za Wa wa Wilaya za Itilima na Meatu ili iweze kutendeka. Mbali na h Serikali imetenga zaidi ya sh milioni 400 kwa ajili ya kuangan wadudu aina ya mbungio ka vijiji vyote vinavyopakana na W Makao na maeneo mengine n ili kutokomeza kabisa mdudu hatari kwa mifugo



**Wananchi wa Kijiji cha Mwangudo wilayani Meatu kinachopakana na Hifadhi ya Jamii ya Makao pamoja na Pori la Akiba la Maswa, wakisalimiana na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina aliyefika kijijini hapo kutangaza maamuzi yaliyotolewa na Rais Dkt. John Magufuli kuhusiana na matumizi ya mita 500 kando mwa hifadhi hiyo kutumika kwa shughuli za malisho ya mifugo.** (Na Mpigapicha Wetu)

# Uchunguzi wa mgon na mifupa kufanyika D

**Na Mwandishi Wetu**

MTAALAMU wa magonj ya uti wa mgongo na mifupa kutoka nchini India anatarajiw kutua nchini wiki hii kwa ajili y kuwafanyia uchunguzi watu mbalimbali wenye matatizo y hiyo.

Uchunguzi huo wa siku m utafanyika katika hospitali ya Regency iliyoko mtaa wa Al jijini Dar es Salaam kwa kus na HCG Multi-Super Speci iliyoko mji wa Ahmedabad r India.

Kwa mujibu wa taarifa ya hospitali ya Regency, uchu huo utafanyika kuanzia Feb na 22 , mwaka huu watu w

# 'Tumieni mbegu bora za miwa zilizofanyiwa tafiti'

Scanned by CamScanner